# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

***Na.18: Msimu wa Kilimo 2025/26*** ***Tathmini ya Machi 21-31, 2026 na Matazamio kwa Kipindi cha Aprili 1-10, 2026***


**MUHTASARI**

- Mvua zinazotarajiwa katika maeneo mengi ya nchi zitaimarisha unyevu wa udongo, hivyo kusaidia katika ukuaji wa mazao na upatikanaji wa malisho, ingawa maji kutuama yanaweza kujitokeza katika baadhi ya maeneo.
- Mazao yanatarajiwa kuendelea kukua vizuri katika maeneo menginchini , hivyo wakulima wanashauriwa kuendelea na shughuli za mashambani kama vile palizi.
- Wakulima na wadau wa kilimo wanashauriwa kushirikiana na maafisa ugani katika maeneo yao huku wakiendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2026


Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipungua nguvu. Hali hii ilisababisha ukanda mvua kusogea kuelekea kaskazini na kuwepo katika maeneo mengi ya nchi na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika baadhi ya maeneo. Aidha, uwepo wa upepo wa bahari wenye unyevunyevu uvumao kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani uliimarisha zaidi mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya pwani ya nchi yetu na yale ya nyanda za juu za kaskazini-mashariki. Vilevile, mifumo ya hali ya hewa katika ukanda wa Ziwa Victoria iliimarika, hali iliyochangia kuongezeka zaidi kwa mvua katika ukanda huo pamoja na maeneo yanayopakana hususan yaliyopo magharibi mwa nchi.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo mengi ya nchi. Pia, vipindi vya mvua kubwa viliripotiwa katika maeneo ya ukanda wa pwani, nyanda za juu kaskazini mashariki na magharibi mwa nchi.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2026

Katika dikadi hii, maeneo mengi ya nchi yalipata jumla ya mvua ya siku kumi kati ya milimita 51 na 100, jambo linaloonyesha mtawanyiko mzuri wa mvua katika sehemu za magharibi, kusini na ukanda wa pwani. Hata hivyo, baadhi ya maeneo ya kanda ya kati na bonde la Ziwa Victoria, hususan maeneo ya Dodoma, Singida, Tabora, Kagera, Shinyanga, Mwanza na Mara, yalipata kiasi cha mvua kisichozidi milimita 50.

Kiwango cha juu zaidi cha mvua katika dikadi hii cha kati ya milimita 201 na 249, kilirekodiwa katika maeneo machache ya kusini mwa mkoa wa Morogoro, kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo.




Kielelezo 1: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Machi 21-31, 2026

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2026

Katika dekadi hii, kiasi cha mvua kilichopatikana katika maeneo mengi ya nchi kiliendelea kuboresha hali ya unyevunyevu wa udongo, jambo ambalo kwa ujumla linachangia kukuza ukuaji wa mazao. Hata hivyo, maji kutuama yameripotiwa katika maeneo ya mabondeni, hususan katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Pwani, Morogoro, Shinyanga na Mwanza, ambapo wakulima wanashauriwa kuchukua hatua stahiki za kuimarisha mifereji ya maji mashambani. Katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, hususan ukanda wa pwani ya kaskazini, bonde la Ziwa Victoria na sehemu za nyanda za juu kaskazini mashariki, wakulima wengi waliendelea na shughuli za usimamizi wa

mashamba kama vile palizi. Mvua zilizopatikana katika baadhi ya maeneo zimesaidia katika hatua za awali za ukuaji wa mazao.

Katika mkoa wa Morogoro, zao la mpunga liliendelea kuwa katika hatua ya kuchanua matawi, na mvua iliyopatikana imesaidia katika ukuaji wa zao hili, hususan katika skimu za kilimo. Wakulima wanahimizwa kuendelea kusimamia vizuri maji mashambani ili kuongeza uzalishaji.

Katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, mazao ya mahindi kwa kiasi kikubwa yaliendelea kuwa katika hatua ya ukuaji wa majani, huku baadhi ya maeneo kama Tabora yakianza kufikia hatua za uzalishaji, ikiwemo hatua ya ukomavu wa nta. Katika mkoa wa Dodoma, mazao ya alizeti na mtama yameripotiwa kutoka katika hatua ya uotaji hadi hatua za awali za ukuaji, yakisaidiwa na mvua iliyonyesha.

Mazao ya kudumu, ikiwemo kahawa katika mikoa ya Kilimanjaro na Songwe, yaliendelea kuwa katika hatua ya kuiva kwa matunda. Kiwango kizuri cha unyevunyevu wa udongo katika kipindi hiki kimekuwa muhimu kwa ukuaji wa matunda, na wakulima waliendelea na shughuli za usimamizi wa mazao.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo na wanyamapori uliendelea kuimarika katika maeneo yaliyopata mvua za kutosha, hali iliyochangia kuboresha afya na hali ya mifugo katika dekadi hii.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2026

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kiliongezeka kiasi hususan kwa maeneo ambayo yaliyokuwa na ongezeko la mvua.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2026

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa Dunia inatarajiwa kupungua nguvu. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua kusogea kuelekea kaskazini na kuendele kuwepo katika maeneo mengi ya nchi na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika baadhi ya maeneo.

Aidha, mifumo ya hali ya hewa inayosababisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka katika misitu ya Congo kuelekea maeneo yaliyopo magharibi mwa nchi, nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa nchi inatarajiwa kuimarisha zaidi mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo hususan katika kipindi cha siku tano za mwanzo za dekadi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2026

Maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria (Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), pwani ya kusini (Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), kanda ya kati (Dodoma na Singida) yanatarajiwa kupata vipindi vya mvua katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajiwa kupata mvua katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), nyanda za juu Kusini-magharibi (Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), kanda ya kusini (Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2026

Hali ya mvua inayotarajiwa katika maeneo mengi nchini itaongeza unyevu nyevu katika udongo na kusaidia ukuaji wa mazao.

**Ushauri:**

- **Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua (kanda ya ziwa Victoria, Pwani ya Kaskazini na Nyanda za juu Kaskazini Mashariki):** Hali ya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi inayotarajiwa zitasaidia katika ukuaji wa wa mazao na shughuli za palizi. Wakulima katika maeneo haya wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo.
- **Maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua (nyanda za juu kusini magharibi, mikoa ya magharibi, Pwani ya kusini na Kanda ya kusini):** Mvua zinazotarajiwa katika maeneo haya zitasaidia ukuaji wa mazao. Wakulima wanashauriwa kufuatlia hali ya mazao na pia kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku.
- **Malisho na upatikanaji wa maji kwa wafugaji:** Wafugaji wanashauriwa kupanda majani ya malisho na kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.
- **Wavuvi wa Samaki baharini na maziwa makuu:** Wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku ili kujua wakati sahihi wa kufanya shughuli za uvuvi kutokana na uwezekano wa kujitokeza mawimbi makubwa na upepo mkali

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2026

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kuimalika kutokana na hali ya mvua inayotarajiwa. Jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo Kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: *www.meteo.go.tz*
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)